# Standard 6 End Term 1 Exam, 2016

## KISWAHILI

MUDA: SAA 1 DAK. 40

**Soma kifungu kifuatavyo. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Mwaka ______1______ kulikuwa na uhaba ______2______ mvua katika sehemu ______3______ za nchi yetu ya kenya. Ukame ______4______ . ulisababisha kuwepo kwa uhaba wa chakula ______5______ . Jambo ______6______ lilifanya ______7______ ya vyakula kupanda. ______8______ ni kawaida ya bei kupanda pindi mazao ______9______ . ______10______ hivyo, mvua ______11______ masika ilipoanza kunyesha, wakulima waliingia mashambani ______12______ . Sasa, mimea ______13______ imenawiri. Tunatarajia mavuno ______14______ mwaka ______15______ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ujao | B. hii | C. uliopita | D. huyo |
| 2. | A. wa | B. ya | C. la | D. za |
| 3. | A. mingi | B. nyingi | C. mwingi | D. wengi |
| 4. | A. haya | B. hili | C. hili | D. huu |
| 5. | A. inchini | B. nchini | C. barani | D. duniani |
| 6. | A. hii | B. hili | C. hiyo | D. huyo |
| 7. | A. bei | B. ghali | C. sababu | D. adhabu |
| 8. | A. Huyu | B. Hivi | C. Hili | D. Hii |
| 9. | A. yaliyopungua | B. yakipungua | C. yanayopungua | D. yanapoangua |
| 10. | A. Hata | B. kama | C. Ingawa | D. Pengine |
| 11. | A. wa | B. ya | C. za | D. mwa |
| 12. | A. pao | B. lao | C. zao | D. yao |
| 13. | A. zingi | B. nyingi | C. mingi | D. wenyi |
| 14. | A. mingi | B. nyingi | C. wengi | D. mengi |
| 15. | A. hii | B. huu | C. hili | D. hizi |

**Kutoka swali la 16,30, chagua jibu kulingana na maagizo**

16. **Andika katika wingi**

    Kalamau yangu ndiyo nzuri

    A. Kalamu yangu ndiyo nzuri.

    B. Kalamu yetu ndiyo nzuri.

    C. Kalamu zangu ndizo nxuri.

    D. Kalamu zetu ndizo nzuri.

17. Karatasi imeraruka.

    A. Karatasi zimeraruka.

    B. Makaratsi zimeraruka

    C. Makaratasi yameraruka

    D. Makaratsi imeraruka

**Kamilisha methali**

18. Fahari wawili wapiganapo ____

    A. adui hufurahi

    B. nyasi huumia

    C. vita hupamba moto

    D. watu hula nyama

19. Aibu ya maiti aijuaye ______

    A. mwosha

    B. kaburi

    C. kifo

    D. daktari

**Kamilisha tashbihi**

20. Mwoga kama ________

    A. mwanamke B. kunguru

    C. kinyonga D. mtoto

21. Nono kama __________

    A. ng'ombe B. ngoima

    C. samaki D. fisi

**Kamilisha tanakali za sauti**

22. Mwalimu alipoingia darasani tulinyamaza ____

    A. ndi! B. mno!

    C. zi! D. ji!

23. Mtoto aliteleza ______

    A. pa!

    B. prrr!

    C. tele!

    D. chumbwi!

**Kanusha sentensi zifuatazo**

24. Nilicheza nikachoka.

    A. Nimecheza sijachoka

    B. Sikucheza sikuchoka

    C. Sikucheza na sikuchoka

    D. Sikucheza wala sikuchoka

25. Nimekula nikashiba.

    A. Nimela nimashiba.

    B. Sijala wala kushiba.

    C. Nimela wala sijashiba.

    D. Nimela nikashiba.

26. Kidonda kisichopona huitwa ______

    A. kidonda ndugu

    B. ugonjwa

    C. uwele

    D. uchungu

27. Jina lenye maana sawa na **mchukuzi** ni ______

    A. mchuuzi

    B. mpagazi

    C. bebabeba

    D. mkokoteni

28. Ni ipi si-ala ya muziki?

    A. Zumari B. Marimba

    C. Tari D. Sime

29. Neno **nywele** liko katika ngeli ipi?

    A. I - ZI

    B. LI - YA

    C. I - I

    D. U - ZI

30. Msimu wa baridi kali bila mvua huitwa ______

    A. masika B. kipupwe

    C. vuli D. matlai

**Soma ufahamu kisha ujibu maswali 31-40**

Ilikuwa ni siku kuu ya mji. Watu wa wilaya ya Hafla walikuwa wakisherehekea siku ya kuanzishwa kwa wilaya hiyo. Wananchi wote wa wilaya hiyo walihudhuria. Kulifanywa karamu kubwa watoto wa shule zote za wilaya hiyo walihudhuria. Waliimba nyimbo tamutamu. Pia kulikuwa na ngoma za kienyeji. Siku hiyo ilikuwa ya furaha tele. Watu walikuwa wakicheza huku wameshikilia wanyama. Walikuja na mbuzi na kondoo. Viongozi wote walihutubia wananchi. Kila aliyesimama aliwahimiza wananchi wawe na amani.

Watoto wa shule waliimba nyimbo nzuri zana. Hata mgeni wa heshima alisimama na kucheza pamoja na watoto hao. Watoto nao walipewa zawadi. Baadaye karamu ilianza. Watu walikula na kunywa kwa furaha.

Mwisho watu wote waliondoka wakiwa na furaha. Watoto waliondoka huku wakiimba nyimbo za kupendeza. Walishukuru kwa zawadi walizopewa.

---

31. Wilaya ya Hafla ilikuwa ikisherehekea_____
    A. kuanzishwa kwake
    B. amani
    C. nyimbo
    D. micheza
32. Watoto wa shule walishiriki katika sherehe kwa ________
    A. kucheza michezo ya kuigiza
    B. kuwatumbuiza
    C. kuwakaribisha wageni
    D. kupokea zawadi
33. Sherehe hizi ziliongozwa na nani?
    A. Mwalimu mkuu
    B. Mgeni mheshimiwa
    C. Chifu
    D. Wanafunzi
34. Ni wanyama gani waliotajwa katika taarifa?
    A. Kuku na mbuzi
    B. Kondoo na mbwa
    C. Mbuzi na ng'ombe
    D. Kondoo na mbuzi
35. Nyimbo zilizokuwa zikiimbwa zamani sana huitwa ________
    A. nyimbo za zamani
    B. nyimbo za wazee
    C. nyimbo za kitamaduni
    D. nyimbo za kishamba
36. Jina jingine la sherehe ni ________
    A. mlo
    B. maakuli
    C. karamu
    D. kalamu
37. Maneno ambayo hunenwa na mgeni wa heshima katika sherehe huitwa______
    A. mahubiri
    B. hotuba
    C. taarifa
    D. msomo
38. Ili kuonyesha adabu, watoto walipopewa zawadi walisema_______
    A. kunradhi
    B. makiwa
    C. tafadhali
    D. shukrani
39. Viongozi waliwahimiza wananchi kufanya nini?
    A. Kusherehekea siku zote
    B. Kudunisha amani
    C. Kufanya kazi kwa bidii
    D. Kudumisha amani
40. Ni kweli kusema kuwa sherehe hii_____
    A. haikufana
    B. ilihuzunisha
    C. ilifana sana
    D. ilichosha

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Kiboko, Sungura na Ndovu walikuwa marafiki wakubwa. Marafiki hawa watatu waliishi kando ya ziwa Bogoria. Siku moja walikuwa na ugomvi wa ni nani aliyekuwa na nguvu zaidi. Basi wote wakaona ni bora washindane. Wakachukua kamba ndefu ili washindane kwa kuivuta. Sungura aliingia ndani ya ziwa hali ameshikilia hiyo kamba akamwambia Kiboko aanze kuivuta baada ya dakika tano. Sungura aliingia ndani ya ziwa na kufunga ile kamba kwenye jiwe kubwa. Baada ya dakika tano Kiboko akaanza kuvuta. Alivuta kwa nguvu mpaka akashindwa. Akamwita Ndovu naye aje avute. Ndovu alivuta pia naye akashindwa. Ndovu na Kiboko walivuta hiyo kamba pamoja, pia wakashindwa.

Ndovu na Kiboko walimwita Sungura nje ya maji na wakakubali ya kwamba alikuwa na nguvu kuliko wao wote. Ndovu na Kiboko walikubali kufanya Sungura awe mfalme wao.

41. Akina Sungura waliishi wapi?
 A. Karibu na msitu
 B. Karibu na ziwa
 C. Karibu na mto
 D. Karibu na bahari

42. Wanyama hawa walitaka kujua aliyekuwa na ___ zaidi.
 A. ujanja
 B. akili
 C. nguvu
 D. werevu

43. Ni kweli kusema kuwa ________
 A. Sungura alikuwa na nguvu kuliko wote
 B. Ndovu ndiye aliyekuwa na nguvu
 C. Kiboko alikuwa na nguvu
 D. Hatujui aliyekuwa na nguvu

44. Nani alikuwa ndani ya maji?
 A. Sungura
 B. Kiboko
 C. Ndovu
 D. Wote

45. Nani alishindana na Sungura kwanza ______
 A. Sungura
 B. Ndovu na Kiboko
 C. Kiboko
 D. Ndovu

46. Nani alituzwa kuwa mfalme?
 A. Sungura
 B. Kiboko
 C. Ndovu
 D. Fisi

47. Sungura alifunga kamba wapi?
 A. Kwenye mti
 B. Kwenye papa
 C. Kwenye nyangumi
 D. Kwenye jiwe

48. Kati ya wanyama hawa nani mkubwa zaidi?
 A. Sungura
 B. Kiboko
 C. Ndovu
 D. Hakuna

49. Sungura alionyesha ______
 A. nguvu zake
 B. upumbavu wake
 C. ujanja wake
 D. ujinga wake

50. Ni methali gani inafaa kifungu hiki?
 A. Akili ni mali
 B. Akili nyingi huondoa maarifa
 C. Mwenye nguvu mpishe
 D. Dawa ya moto ni moto